Australian Government
AUSTRAC

FIGHTING FINANCIAL CRIME TOGETHER

# Kutambua wateja binafsi
## Taarifa muhimu kwa watoa huduma za kifedha

### Ni wakati gani nahitaji kumtambua mteja?

Lazima uangalie kitambulisho cha mteja kwa kukusanya na kuthibitisha habari **kabla** ya kutoa huduma zozote zilizotengwa kwao. Hii inajulikana kama kitambulisho cha mteja, au Jua Mteja wako (KYC).

Baada ya kuangalia kitambulisho cha mteja, lazima uridhike kuwa mteja ndie anaejitambulisha kuwa.

Katika kila kisa, unapaswa pia kutumia busara yako mwenyewe ikiwa utatoa huduma kwa mteja kulingana na tathmini yako ya hatari ya mteja huyo na muamala.

### Ninamtambuaje mteja binafsi?

Kuna hatua mbili za kukamilisha utambulisho wa mteja

1. **Chukua** taarifa za kitambulisho kutoka kwa mteja
2. **Thibitisha** taarifa za kitambulisho cha mteja dhidi ya vyanzo vya kuaminika na huru.

Unaweza kutumia hati za kuaminika na huru au data ya elektroniki (au zote mbili) ili kuthibitisha taarifa za mteja

### Ni taarifa gani ninahitaji kukusanya na kuthibitisha kwa wateja binafsi?

| WATEJA BINAFSI (SIO MFANYABIASHARA) | | |
|---|---|---|
|  | **Kusanya** | Lazima ukusanye zifuatazo:<br>• Jina kamili la mtu huyo<br>• Anwani ya makazi<br>• Tarehe ya kuzaliwa |
| | **Thibitisha** | Lazima uhakikishe taarifa zifuatazo:<br>• Jina kamili la mtu huyo, **NA**<br>• Ama anwani ya makazi au tarehe ya kuzaliwa |

| MFANYABIASHARA (ANAYEFANYA KWAJIRI YA BIASHARA) | | |
|---|---|---|
|  | **Kusanya** | Lazima ukusanye taarifa zote zifuatazo:<br>• Jina kamili la mtu huyo<br>• Jina kamili la biashara ambalo mteja hutumia kufanya biashara yake (ikiwa inahitajika)<br>• Nambari ya Biashara ya Australia (ABN) (ikiwa inahitajika)<br>Lazima kukusanya moja ya taarifa zifuatazo:<br>• Anwani ya makazi, **AU**<br>• Anwani ya mahali kuu pa biashara (ikiwa inahitajika) |
| | **Thibitisha** | Lazima uhakikishe taarifa zifuatazo:<br>• Jina kamili la mtu huyo, **NA**<br>• Ama anwani ya makazi au tarehe ya kuzaliwa |

## Nyaraka za utambulisho

| Mifano ya nyaraka za utambulisho | |
|---|---|
| **Nyaraka za msingi za utambulisho** (zilizotolewa na serikali) | Leseni ya dereva au kibali kutoka Australia au ng'ambo (pamoja na leseni ya dereva ya kidijitali) |
| | Hati ya kusafiria ya Australia |
| | Kadi ya serikali ya thibitisho la umri iliyotolewa Australia |
| | Hati ya kusafiria ya kigeni iliyotolewa na serikali ya kigeni au Umoja wa Mataifa |
| | Nyaraka za kusafiri za kimataifa zilizotolewa na serikali ya kigeni au Umoja wa Mataifa |
| | Kitambulisho cha kitaifa kilichotolewa na serikali ya kigeni au Umoja wa Mataifa |
| | Cheti cha kuzaliwa cha Australia, dondoo ya kuzaliwa au cheti cha uraia |
| | Cheti cha kuzaliwa cha kigeni au cheti cha uraia |
| | Kadi za idhini zilizotolewa na serikali, kama kadi ya idhini ya wastaafu, kadi ya utunzaji wa afya, au kadi ya utunzaji ya wazee |
| | **Kumbuka:** Ikiwa hati ya kusafiri au kitambulisho kipo katika lugha ya kigeni, na mtu anayehakikisha hati hizo haelewi lugha ya kigeni iliyotumiwa, mteja lazima atoe tafsiri ya Kiingereza iliyoidhinishwa. |

| | |
|---|---|
| **Nyaraka za ziada za utambulisho** | Notisi kutoka kwa Ofisi ya Kodi ya Australia au wakala mwingine wa serikali, kama vile Centrelink, ambayo ina jina la mtu binafsi na anwani ya makazi - iliyotolewa katika miezi 12 iliyopita |
| | Notisi ya viwango vya baraza la manispaa au bili ya huduma (kama bili ya maji, gesi au umeme) ambayo ina jina la mtu na anwani ya makazi - iliyotolewa katika miezi mitatu iliyopita |
| | Kwa mtu mwenye umri chini ya miaka 18, barua kutoka kwa mkuu wa shule - iliyotolewa katika miezi mitatu iliyopita - yenye maelezo ya jina la mtu, anwani ya makazi na wakati aliohudhuria shule, au kadi ya mwanafunzi ikiwa inapatikana. |

### Takwimu za elektroniki

Lazima uzingatie ikiwa data ya elektroniki ni ya kuaminika na huru ikiwa unathibitisha maelezo ya wateja kwa njia hii. Kuamua ikiwa nyaraka ni za kuaminika na huru, angalia **austrac.gov.au/verify**

### Wateja wenye hatari kubwa na ukaguzi wa kina wa mteja.

Unapotathmini mteja ama muamala kuwa na hatari kubwa, lazima ufanye ukaguzi wa kina wa mteja, au ECDD. ECDD inaweza kuhusisha ukaguzi wa ziada wa utambulisho wa mteja, kukusanya taarifa za ziada na kufanya uhakiki wa ziada. Kutambua ni wakati gani wa kutumia ECDD yako, angalia **austrac.gov.au/ECDD**

### Watu wanaofahamika kisiasa.

Mtu anaefahamika kisiasa, au PEP, ni mtu ambaye ana wadhifa maarufu kwenye umma au nafasi katika mwili wa serikali au shirika la kimataifa, iwe Australia au ng'ambo. Wanafamilia wa karibu na washirika wa karibu wa watu hawa pia huchukuliwa kama PEPs. Kutambua na kukamilisha utambulisho wa mteja kwa PEPs, angalia **austrac.gov.au/PEPS**

### Hali maalum: Wateja wasio na vitambulisho vya kawaida

SWateja wengine wanaweza wasiwe na aina za kawaida za vitambulisho. Unaweza kupata orodha ya aina zingine za vitambulisho kwenye wavuti ya AUSTRAC. Kutambua wateja hawa, angalia **austrac.gov.au/identity**

### Taarifa zaidi

Kwa maelezo zaidi juu ya majukumu ya KYC, au kwa taarifa juu ya mahitaji ya wateja wa aina mbalimbali, angalia **austrac.gov.au/KYC**

**Tahadhari**

Taarifa iliyomo kwenye waraka huu inakusudiwa kutoa muhtasari tu na mtazamo wa jumla. Haikusudiwa kuwa ya kina. Haijumuishi wala haipaswi kutumika kama ushauri wa kisheria. Jumuiya ya Madola haikubali dhima kwa hasara yoyote iliopatikana kutokana na kutegemea waraka huu. Kabla ya kufanya uamuzi au kuchukua hatua fulani kulingana na yaliyomo kwenye waraka huu, unapaswa kuangalia usahihi wake, ukamilifu, sarafu na uwiano kwa madhumuni yako. Unaweza kutaka kutafuta ushauri wa kitaalam wa kujitegemea.

© Copyright Commonwealth of Australia

